- **Maonyesho ya Swahili Fashion Week kufanyika November 30 hadi Disemba 2 mwaka huu**
- **Maonyesho ya Swahili Fashion Week 2018 kusisitizia sera ya uchumi wa viwanda**
- **Zaidi ya wabunifu 50 kushiriki katika maonyesho ya Swahili Fashion Week 2018**
- **Balozi wa Italia nchini azindua nebo mpya ya Swahili Fashion Week 2018**

Wiki ya maonyesho ya jukwaa la mitindo la kipekee Afrika mashariki na kati kufanyika tarehe Novemba 30 hadi Disemba 2 mwaka huu katika eneo la Makumbusho ya Taifa (Posta) jijini Dar es Salaam. Huku mandaalizi yakiwa ya kusisimua na kufurahisha sababu tupo tayari kuwasilisha "**Kungundua kile kinachofanya Afrika kuwa Nzuri**" na kuonyesha kazi za mitindo zilizo katika hali ya juu kwa wadahu wote wa sekta ya mitindo.

Katika kuendeleza mafanikio makubwa na yakipekee kwa misimu 10 iliyopita, maonyesho ya Swahili Fashion Week na tuzo yanaendelea kuwa jukwaa bora na lenye ushawishi mkubwa zaidi kwa afrika katika kuimarisha teknolojia ya sekta ya mitindo, kukuza vipaji bora, kuhamasisha ubunifu wa mitindo na kujivunia tamaduni za Kiswahili.

Mwanzilishi wa jukwaa mashuhuri la mitindo la Afrika mashariki na Kati, kwa utiifu wote anasema "lengo la kundeleza na kuhimarisha nafasi ya mitindo kwa Afrika linabaki kuwa mbele, kupitia jukwaa hili na mchango mkubwa wa waandishi wa habari tutaendelea kuunga mkono vipaji vilivyopo katika sekta ya mitindo tukiwa tunaweka alama ya msimu wa kumi na moja wa maonyesho ya Swahili fashion week, tunafurahi kuona tunayaendea malengo yetu tuliyoyaweka wakati tulipoanzisha maonyesho haya ya kifahari kwa kujiamini"

Mustafa aliongeza kuwa " malengo katika Sekta ya mitindo Tanzania ni kuwa na uwezo wa kutengeneza na kuuza katika soko la kimataifa, ndio sababu onyesho la Swahili fashion week linaunga mkono katika kutekeleza juhudi za Raisi wa Jamuri ya Muungano wa Tanzania Dkt.John P Magufuli katika sera ya kuelekea uchumi wa viwanda kupitia bidhaa za nguo "**zilizotengenezwa Tanzania** ", kama alivyosema katika hotuba yake ya utambulisho mwaka 2015. Hivyo basi, tunawaomba vyombo vya habari na wadau wengine kusherekea nasi kwa kuwaunga mkono wabunifu wetu wa mitindo na kushuhudia mitindo ya kipekee katika maonyesho haya. Kama methali hii ya Afrika inavyosema "kama unataka kwenda haraka nenda mwenyewe, kama unataka kwenda mbali nenda pamoja"

Msimu wa kumi na moja wa maonyesho ya Swahili Fashion Week, utakuwa wa kipekee na kuendelea kuwa kivutio katika maonyesho yote ya mitindo nchini Afrika, pamoja na wabunifu wa ndani na kimataifa wakipata hisia za dhati kutoka kwa vyombo vya habari vya nchini na nje ya nchi toka maonesho haya yalipoanzishwa mwaka 2008. Swahili fashion week limekuwa jukwaa la kwanza lenye ubunifu kwa wabunifu wa mitindo kutoka Afrika Mashariki na kwengineko ambao uonyesha mavazi yao kwa ulimwengu kwa wakati mmoja.

Katika kusherehekea awamu ya kumi na moja ya maonyesho haya, miongoni mwa vitu ambavyo tunangazia ni kutilia mkazo ukuaji wa tamaduni za Kiswahili hasa lugha ya Kiswahili. Maonyesho ya Swahili Fashion Week hayakuzi lugha ya mazungumzo pekeake pia ukuza lugha ya vitendo kupitia mavazi ya ubunifu. Hii ni kwasababu lugha ya Kiswahili uzungumzwa na watu zaidi ya milioni 100 barani Afrika na ni lugha inayojulikana na kutumika kama lugha ya kurushia vipindi katika na mashirika ya kimataifa ya vyomba vya habari. Vilevile nchi kadhaa barani Afrika imekipa nafasi lugha ya Kiswahili kama chombo cha tamaduni za kidiplomasia " alisema Meneja wa Mradi wa Swahili Fashion Week ,Glory Urassa

Uzinduzi wa Swahili Fashion Week ulipata baraka kutokana na uwepo wa Balozi wa Italia nchini Tanzania Mh.Roberto Mengoni, alisema "Sekta ya mtindo nchini Italia imekuwa ni mwajiri mkubwa katika nchi yao, na kutoa kazi 350,000 na kuongeza pato la zaidi ya bilioni 15 kwa mwaka jana, kwa hiyo natumaini sekta ya mtindo wa Tanzania itapanuka pia na kuweza kuchangia katika uchumi wa Tanzania. Ubalozi wa Italia nchini Tanzania umesaidia

sana maonyesho haya na tunaahidi kuunga mkono wabunifu wa hapa nchini ili kufikia soko la kimataifa "

Mwaka huu maonyesho ya Swahili Fashion Week na Tuzo yatafanyika kuanzia Novemba 30 hadi Disemba 2 katika ukumbi wa Makumbusho ya Taifa, yakiwa na wabunifu Zaidi ya 50 kutoka nchini na nje ya nchi. Nyakati za jioni kuanzia saa kumi jioni hadi saa nne usiku kutakuwa na bazaar na muziki wa bandi, wajasiliamali mbalimbali wataonesha bidhaa zao za kazi za mikono, Sanaa na vito, sambamba na sehemu ya mapumziko kwa watu maalum itakuwepo kwa wale wanaotaka kutumia jioni yao wakiwa pamoja na watu maarufu, watu wa mitindo na vyombo vya habari huku wakiburudika na maonyesho makubwa ya mitindo Tanzania.

Maonyesho ya Swahili Fashion Week yameandaliwa na 361 Degrees Africa na kudhaminiwa na Ubalozi wa Italia Tanzania, Golden Tulip Hotel City Centre, BASATA, Asila's Makeup, Nexia SJ, GreenTelecom, Epidor, Michuzi Blog , Aim Group, Spik and Span na Uber Tanzania.

KUHUSU SWAHILI FASHION WEEK

Swahili fashion week ni onyesho kubwa la mitindo na mavazi afrika mashariki na kati linaliofanyika kila mwaka, ni jukwakaa kubwa linalowapatia nafasi wabunifu wa mavazi na vito kutoka nchi za afrika masharika na zinginezo kuonyesha vipaji vyao, kutengeneza soko la ubunifu na kupata na kukuza mtandao wa wateja katika tasnia ya mitindo.

onyesho hili lina nia ya kusisitiza jamii kuwa mitindo ni pato linalozalisha tasnia ya ubunifu, wakati huo huo ikikuza dhana ya "bidhaa za afrika ". Swahili fashion week ni jukwaa la mitindo lilianzishwa mwaka 2008 na Mustafa Hassanali mbunifu kubwa na mkongwo afrika kutoka Tanzania.

Swahili Fashion Week ni jukwaa la mitindo lilianzishwa mwaka 2008 na mbunifu mkongwe na mashuguhuli kutoka Tanzania, Mustafa Hassanali

Onyesho la mwaka huu litakuwa onyesho la 11 toka lianze kufanyika.

Media Inquiries

Maryam@361africa.com

+255785862323